JARIDA KUHUSU |UTALII | UHIFADHI NA MASUALA MBALIMBALI

# TZ&BEYOND

SEPT, 2025 |ISSUE NO 19 TSHS.20,000 KSHS.1,187 USHS 30,000 | ISSN 2799-225X |LESENI 00000021


Multisectoral magazine



# 2025

## ANATOSHA MITANO TENA

| | | |
|---|---|---|
| AMEFANYA MAMBO MAKUBWA NDANI YA MUDA MFUPI | AMELETA MABADILIKO MAKUBWA KATIKA ELIMU AFYA,UTALII MAJI,BARABARA,NISHATI, MICHEZO NA AJIRA KWA WATANZANIA | WANANCHI WASOMI, WENASIASA, VIONGOZI WA DINI WAMWAGIA SIFA |




# Experience the power of TemboCARD

Shop locally and internationally at over 44 million merchants and 2 million ATMs

VISA

CRDB BANK

*The bank that listens*


# BODI YA WAHARIRI

**AFISA MTENDAJI MKUU**
JIMMY C. KIANGO
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MHARIRI MTENDAJI**
JIMMY C. KIANGO
Cell: 0787 180 065
jimmy.kiango@tz&beyond.co.tz

**MHARIRI:**
SIDI MGUMIA
Cell: 0714327572
mgumia.sidi@tz&beyond.co.tz

**MENEJA WA IT**
FELIX JIMMY ALOYCE
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MSANIFU KURASA MKUU**
FELIX JIMMY ALOYCE
Cell: 0763 520 319
felix.aloyce@tz&beyond.co.tz

**MWANDISHI**
HASSAN DAUD
**Cell: 0692 695 889**
hassan.@tz&beyond.co.tz

**MWENYEKITI**
DK. THOMAS KASHILILAH
[FCLPP, FAAPM CIPM,GAFM, ChE, AFA]
Cell: 0754 997 645
legiconsult@outlook.com

**MLEZI**
NASSIR ABDALLAH
Cell: 0713 767685
nasir.abdallah@panaromanews.co.tz

---


**TZ&BEYOND**
Mbezi Beach Park Building;
Off Bagamoyo Road
P.O. Box 79010, Postcode: 14121
Phone: +255 655 06 38 39
Dar Es Salaam , Tanzania


**MAUZO/MATANGAZO**
Sales Team,TZ&BEYOND
Cell: 0655063839
email: tz1andbeyond@gmail.com




www.tz&beyond.co.tz







17
RAIS SAMIA AMETEKELEZA KWA VITENDO AKAMILISHA ILANI YA CCM ZAIDI YA ASILIMIA 90



47
AMEBORESHA SEKTA YA USAFIRI



24
AMEBORESHA HUDUMA YA AFYA KWA MAMA NA MTOTO



21
MAZINGIRA BORA KWA WACHIMBAJI WA MADINI




22
TRA YAVUKA REKODI ZA MAKUSANYO, SASA YAKUSANYA KODI KIRAFIKI



11
TAMKO LA TANZANIA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA ULAYA



16
ROYAL TOUR YAONGEZA WATALII



14
AMEJENGA MADARASA NA KUONGEZA MIKOPO ELIMU YA JUU



15
AMEUWEZESHA MRADI MKUBWA WA TRENI YA UMEME



19
VIWANDA NA BIASHARA VYACHANGIA ZAIDI YA TRILIONI 20



28
VIWANJA 12 VYA NDEGE VYABORESHWA, NDEGE 11 ZIMENUNULIWA

# TZ&BEYOND



***Jarida hili linalowafikia watu wa rika na kada*** mbalimbali ndani na nje ya Tanzania limelenga kukupa maarifa ambayo huwezi kuyapata kwenye jarida lolote **Tanzania**.

**TZ&BEYOND** limejikita kwenye kuchambua masuala ya siasa, Bunge, Uchumi, Mazingira, Uhifadhi na Habari za kimataifa dhamira yake kuu ni kuwa darasa mikononi mwako.

***TUNA MWANZO, HATUNA MWISHO***

USIKOSE KUSOMA MAJARIDA YETU KUPITIA TOVUTI

www.tz&beyond.co.tz






# UWANJA SAWA WA KISIASA WATAWALA UCHAGUZI MKUU 2025

NA ALLY KAMUMBI

Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 29,2025 unatazamwa kuwa na uwanja saw awa ushindani ikizingatiwa kuwa huu ni uchaguzi wa saba tangu Tanzania irejee kwenye mfumo wa uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1995 ulipofanyika uchaguzi Mkuu wa kwanza uliomwingiza madarakani Hayati Rais Benjamin Mkapa.

Uchaguzi huu unajitokeza katika muktadha wa kipekee wa siasa za Tanzania, uliobeba agenda na sio chuki, ingawa ukweli unasalia kuwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaonekana kuwa na nafasi kubwa zaidi kutokana na kubebwa na dhana ya 'incumbency advantage', iliyotokana na kufanya mambo mengi ya maendeleo yanayowanyima hoja wapinzani wake.

Tayari Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imeshawaingiza wagombea 17 wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulingni, baada ya wagombea hao kutoka vyama 17 kurejesha fomu na kukidhi masharti ya kikatiba na kisheria.

Wagombea waliothibitishwa na Tume ni kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambapo Rais aliyepo madarakani, Dkt. Samia, amethibitishwa kugombea urais akiwa na Balozi Dkt. Emanuel Nchimbi kama mgombea mwenza

Chama Cha Wananchi (CUF) kimemsimamisha Gombo Samandito Gombo akiwa na mgombea mwenza Husna Mohamed Abdalla. NCCR-Mageuzi kitawakilishwa na Haji Ambar Khamis pamoja na Dkt. Eveline Wilbard Munisi, huku chama cha CHAUMMA kikiwasimamisha Salum Mwalimu na Devotha Mathew Minja.

Katika chama cha UDP, mgombea ni Saum Hussein Rashid, mgombea mwenza ni Juma Khamisi Faki. Chama cha TLP amethibitishwa Yustas Mbatina Rwamugira na Amana Suleiman Mzee. Chama cha DP amepitishwa Abdul Juma Mluya akiwa na Sadoun Abrahman Khatib, wakati chama cha TADEA kimemsimamisha Georges Gabriel Bussungu kuwania urais na Ali Makame Issa kama mgombea mwenza.

Kwa upande mwingine, chama cha UMD, Tume imemthibitisha Mwajuma Noty Mirambo akiwa na mgombea mwenza Mashavu Alawi Haji. UPDP amepitishwa Twalib Ibrahim Kadege na Abdalla Mohamed Khamis. NRA ameteuliwa Hassan Kisabya Almas kuwania urais na Hamis Ali Hassan mgombea mwenza, huku chama cha MAKINI kikiwa na mgombea urais Coaster Jimmy Kibonde na mgombea mwenza Azza Haji Suleiman.

Chama cha NLD kitawania urais kupitia Doyo Hassan Doyo pamoja na Chausiku Khatib Mohamed kama mgombea mwenza, wakati SAU kimemsimamisha Majalio Paul Kyara kupeperusha bendera ya chama hicho na Satia Mussa Bebwa. CCK kimempitisha David Daud Mwaijojele na mgombea mwenza Masoud Ali Abdala, huku chama cha AAFP kikiwa na Kunje Ngombare Mwiru kama mgombea urais pamoja na Chumu Abdallah Juma, mgombea mwenza.

Kwa mwaka huu, idadi ya wagombea wa urais imeongezeka hadi 17, ikilinganishwa na wagombea 15 walioteuliwa na Tume ya uchaguzi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Hata hivyo, hakutarajiwi kuwa na ushindani mkubwa, hasa kutokana na kutoshiriki kwa vyama viwili vikubwa vya upinzani, CHADEMA na ACT Wazalendo.

Chadema haishiriki kabisa uchaguzi wa mwaka huu, wakati ACT chenyewe baada ya mgombea wake urais, Luhaga Mpina kuenguliwa, kitashiriki kwenye ngazi ya ubunge na udiwani, na urais kwa upande wa Zanzibar.

Katika uchaguzi wa mwaka 2020, Tume ya uchaguzi ilipitisha wagombea 15 wa urais ambapo Hayati Dkt. John Pombe Magufuli wa CCM aliibuka mshindi kwa kura milioni 12.5, akifuatwa na Tundu Lissu wa CHADEMA aliyepata kura milioni 1.9. Ukiacha Chadema iliyoshiriki, vyama vingine vyote vya upinzani hakuna kilichofikisha kura laki moja.

**KAZI ZA SAMIA NA HOJA ZA WAPINZANI**

Tangu alipoingia madarakani mwaka 2021, Rais Samia amejaribu kujenga urithi wa kisiasa unaojikita katika, Utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya kimkakati (SGR, Bwawa la Nyerere, bandari na barabara), ambayo imejengeka kama alama ya uhalali wa kisiasa (political legitimacy) kwa CCM.

Diplomasia ya kiuchumi inayolenga kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni na kuimarisha taswira ya Tanzania kimataifa.

Mageuzi ya kisiasa yanayoashiria kuimarika kwa demokrasia shirikishi mfano kufanyia kazi mapendekezo ya marekebisho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa.

Ajenda za kijamii zinazojikita katika usawa wa kijinsia, nafasi za vijana, na kuboresha huduma za kijamii.

Kwa upande wa upinzani, hoja kuu zinazojitokeza ni kudai uwajibikaji na uwazi wa kiserikali, hususan katika usimamizi wa miradi mikubwa.

Kuimarisha uchumi shirikishi, ukilenga ajira kwa vijana na uboreshaji wa sekta isiyo rasmi, kuendeleza mjadala wa mabadiliko ya kikatiba ili kujenga mfumo wa kisiasa usioegemea chama kimoja na kuongeza usawa katika huduma za kijamii.

Hata hivyo, changamoto kwa vyama vya upinzani inabaki kuwa ni ukosefu wa mkakati wa pamoja wa kisiasa, jambo linalopelekea ushindani wao kutokuwa na nguvu ya kitaifa.

Aidha vyama vya upinzani kushindwa kuweka wagombea katika majimbo na Kata zote kunaleta ukakasi wa dhamira yao ya dhati ya kutaka kushika dola.

Tangu mwaka 1995, vyama vya upinzani vimekuwa vikikabiliwa na changamoto kadhaa za kimfumo na kimazingira ambazo zimewafanya washindwe kuwasimamisha wagombea katika majimbo yote na kata zote.

Kwa miaka takribani 20 sasa vyama hivyo vimeshindwa kujiimarisha katika rasilimali fedha na watu, gharama za kisiasa na kiuchaguzi ni kubwa, na vyama vya upinzani havina mtaji wa kifedha kulinganisha na CCM.

Pamoja na hilo lakini pia vinakabiliwa na changamoto za kiutawala ndani ya vyama, kumekuwa na migawanyiko ya kiuongozi, urasimu, na mara nyingine migogoro ya kifalsafa.

Ingawa wao wanabeba hoja kuwa mazingira ya kisheria na kisiasa si rafiki kwao kwa hoja kuwa mfumo wa kisheria mathlani gharama za fomu, masharti ya usajili wa wagombea na wakati mwingine vizuizi vya kiutendaji vinavyosababisha wagombea wengi wa upinzani kuenguliwa.



# RAIS SAMIA

## AMETEKELEZA KWA VITENDO

AKAMILISHA ILANI YA CCM ZAIDI YA ASILIMIA

**90**

VISION PLUS
EYE CLINIC



TUNAPIMA MACHO | MIWANI YA KILA AINA




TUNAPOKEA KADI ZA STRATEGIS NA **NHIF** ZA WABUNGE

HUDUMA YA HUHAKIKA

VISION PLUS ZANZIBAR

AFYA HOUSE OPP CLOUDS RADIO
COCA COLA ROAD
TEL: 0778 227 252
ZANZIBAR TUPO
MLANDEGE,BOMBAY BAZAAR


# Q&A

## MSAJILI: JUKUMU LETU NI KULEA VYAMA VYOTE BILA UBAGUZI

Na JIMMY KIANGO

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini ilianzishwa mwaka 1992 kwa mujibu wa sheria ya Vyama vya Siasa namba 5 ya mwaka 1992, ikiwa na majukumu ya kusajili vyama vya siasa, kugawa ruzuku ya serikali kwa vyama vya siasa na kufuatilia mapato na matumizi ya vyama vya siasa.

Kutokana na majukumu hayo na ikizingatiwa kuwa mwaka huu Tanzania itakuwa na Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 29,2025, jarida hili liliiona haja ya kufanya mahojiano na Msajili wa Vyama vya siasa nchini Jaji Francis Mutungi, ambapo Pamoja na mambo mengine alitoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu vyama vya siasa nchini:

**TZ&BEYOND:** Ukiwa ndie mlezi mkuu wa vyama vya siasa nchini, umechukua hatua gani kuhakikisha vyama vinaendesha shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya kidemokrasia na utawala bora?

**JAJI MUTUNGI**: Ofisi yangu imekuwa ikiendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa viongozi wa Vyama vya Siasa ili kuvijengea uwezo wa kuendesha vyama vyao kwa mujibu wa Sheria. Na hivi karibuni tumemaliza mafunzo kwa viongozi wa vyama yaliyotolewa kwa viongozi wa vyama walioko Zanzibar na wale walioko Tanzania Bara ili kuwandaa kwa zoezi la Uhakiki.

Vile vile kila mwaka kwa mujibu wa Sheria, Ofisi imekuwa ikiendesha zoezi la Uhakiki wa vyama vya siasa kwa dhumuni la kuhakikisha Vyama vya Siasa vinajiendesha kwa kufuata Sheria zinazosimamiwa na Ofisi yetu lakini pia vikizingatia sheria zingine za nchi, maadili na misingi ya utawala bora katika shughuli zao za kila siku.

**TZ&BEYOND:** Je, ofisi yako imepokea taarifa au malalamiko rasmi kutoka kwa vyama vya siasa kuhusu changamoto zozote zinazokwamisha mageuzi ya kisiasa nchini?

**JAJI MUTUNGI:** Ndiyo, kama Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, tumepokea taarifa na malalamiko rasmi kutoka kwa baadhi ya vyama vya siasa kuhusu changamoto mbalimbali zinazodaiwa kukwamisha mageuzi ya kisiasa nchini. Taarifa hizo zimepokelewa kwa njia mbalimbali kama maandishi, mikutano rasmi, au kupitia majukwaa ya kisiasa kama Baraza la Vyama vya Siasa.

Baadhi ya changamoto zilizoripotiwa na vyama ni kama mgawanyo wa Ruzuku, ambapo baadhi vyama visivyopata mgao vinalalamika kutopata ruzuku kunaathiri utendaji wao wa kazi wa kila siku.
Pia kupitia Baraza la Vyama vyama vya Siasa, Ofisi imepokea malalamiko kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa 2024. Huku wakitoa mifano kwa uchaguzi mkuu wa 2020 na 2019 kwamba chaguzi zote hizo zilikuwa na kasoro kadhaa.

Malalamiko yao ni kuhusu mifumo ya uchaguzi, ambayo kwa namana moja au nyingine serikali imeshachukua hatua kwa kiasi kikubwa kwa kutungwa upya kwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani na pia ili kuboresha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa imeshaamuliwa kwamba mara baada ya kutungwa Sheria rasmi, uchaguzi huo wa Serikali za Mitaa utaanza kusimamiwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi.

Kwa kuziona changamoto hizi, Ofisi yangu imechukua hatua mbalimbali kama kuratibu majadiliano katika makongamano makubwa ya wadau wa deomokrasia nchini na vikao vya Baraza la Vyama vya Siasa, yote imekuwa ikijadili changamoto hizo na kutafuta suluhisho la pamoja na kuwasilisha mapendekezo serikalini.
Aidha, Ofisi yangu imekuwa ikihamasisha ushirikishwaji wa wanawake na makundi maalum katika shughuli za vyama vya siasa.

**TZ&BEYOND:** Kwa mujibu wa tathmini yako, ni matatizo gani makuu yanayovikumba vyama vya siasa nchini na unaamini yanasababishwa na nini?

**JAJI MUTUNGI:** Zipo changamoto kadhaa, lakini kubwa kabisa ni ukosefu wa rasilimali fedha. Hiyo ni changamoto kubwa. Kutokuwepo kwa vyanzo mbadala vya mapato kunafanya vyama vishindwe kuendesha shughuli mbalimbali kama kushiriki vyema katika uchaguzi na hata kuendesha ofisi zao.
Kitu kingine ni kuminywa kwa demokrasia kwa baadhi ya vyama vya siasa, suala hili tunalifanyia kazi kwakuwa huwa tunafuatilia mikutano ya uchaguzi ya vyama hivyo.

Changamoto nyingine ni uwepo wa migogoro ya ndani ya baadhi ya vyama vya siasa. Migogoro hiyo



NI KINARA WA MAENDELEO, ANATOSHA AFANYA MAPINDUZI MAKUBWA KWENYE ELIMU, AFYA, MIUNDOMBINU, UMEME, MAJI, UTALII, BANDARI NA MAKUSANYO YA KODI



# RAIS SAMIA

## AMETEKELEZA KWA VITENDO

AKAMILISHA ILANI YA CCM ZAIDI YA ASILIMIA

# 90

NA JIMMY KIANGO

Watanzania wengi wa mijini na vijijini wanamtazama Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama mwanamke shupavu, hodari na mwenye huruma, ambae ameonesha kwa vitendo ni kwanini mwaka 2015 na baadae mwaka 2020 aliaminiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea mwenza kwenye uchaguzi Mkuu uliomwingiza madarakani, Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, 2021. Wakati Hayati Magufuli akiwa Rais,Dkt. Samia alikuwa ndie Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke tangu Tanganyika na baadae Tanzania ipate uhuru wake Desemba 9,1961.

Kufariki kwa Magufuli ikiwa ni mara ya kwanza kwa Tanzania kukumbwa na dhahama hilo la Rais kufia madarakani, kuliilazimisha mihimili ya dola kurejea kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuangalia nini kinapaswa kufanyika na nchi iendelee kuwa katika mikono salama.

Hatimae nchi ikasimama kwenye Ibara ya 37(5) ya Katiba inayoelekeza wazi kuwa: Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kutokana na Rais kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi ya mwili au kushindwa kuetekeleza kazi na shughuli za Rais basi Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano...

Hatua hii ilipokelewa kwa shangwe na Wananchi wengi, hata hivyo wapo baadhi ya watu wenye nia ovu na nchi, walitilia shaka jinsi ya kike wakidhani kuwa mwanamke hawezi kuongoza nchi.

Katika kuwadhihirishia kuwa yeye si mwepesi kama walivyokuwa wakidhani wakosoaji wake, Machi 22,2021 akitoa salamu zake kwa umma katika maombolezo ya kitaifa ya Hayati Magufuli aliwaeleza wazi kuwa yeye ndie Rais.
“Mimi ndie Rais, kwa wale ambao wana mashaka na mwanamke huyu ataweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Nataka niwaambie aliyesimama hapa ni Rais, nataka nirudie, aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambae maumbile yake ni mwanamke.”

Kauli hiyo ya kishujaa ilimaliza fikra na mawazo ya harakati ovu dhidi ya Rais Samia na hapo ndipo alipodhihirisha kuwa ni mwanamke shupavu na hodari.
Hakuna shaka yeyote, Rais Dkt. Samia ameweza, anaweza na sasa watanzania wengi wanasema wazi kuwa anatosha na kustahili kuliongoza taifa hili kwa miaka mitano mengine.

Katika kipindi chake cha miaka minne ya uongozi wake amefanya mambo makubwa na mazito ambayo yamewaziba midomo wakosoaji wake na kusalia na malalamiko yasiyo na tija.

Rais Dkt. Samia ameweza kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na CCM kupitia Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha miaka minne sanjari na mpango wa maendeleo miaka mitano.

Ikumbukwe kuwa katika ilani hiyo, chama kimeelekeza Serikali kutekeleza masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiulinzi na kiusalama, na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa ajili ya ustawi wao na Taifa kwa ujumla.

Katika jitihada za kuhakikisha maelekezo hayo yanatekelezwa kikamilifu na kwa wakati, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji huo kwa kishindo.
Mafanikio makubwa yamepatikana ikiwemo kuongezeka kwa Pato la Taifa kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.1 mwaka 2023 na ilitazamiwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka huu wa 2025.

Mfumuko wa bei wa Taifa umeshuka na kufikia asilimia 3.0 Novemba, 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.1 Novemba, 2020.

Mfumuko wa bei ulio katika tarakimu moja umechangia kuwa na utulivu wa thamani ya shilingi, kuongezeka na kuimarika kwa kiwango cha uzalishaji na kukua kwa uchumi na ustawi wa jamii.

Serikali ya Rais Dkt. Samia imechukua hatua mbalimbali ili kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo afya, maji na elimu.

## RAIS SAMIA AMETEKELEZA KWA VITENDO AKAMILISHA ILANI YA CCM ZAIDI YA ASILIMIA 90

### SEKTA YA AFYA
Katika sekta ya afya, hatua hizo zilijumuisha ujenzi wa majengo ya kutolea huduma, upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa tiba na mitambo ya kisasa ya uchunguzi na ugunduzi wa magonjwa pamoja na kuhamasisha jamii kuzingatia masuala ya lishe hasa kwa watoto walio chini ya miaka mitano.

### SEKTA YA ELIMU
Kwa upande wa elimu, Rais Samia ameendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada katika ngazi ya shule za msingi na sekondari, kujenga na kukarabati miundombinu ya shule nchini, kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu pamoja na kuhuisha mitaala mbalimbali ya elimu.













### SEKTA YA MAJI
Kwa upande wa sekta ya maji, Serikali imesimamia utekelezaji wa sera, mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, kuendeleza tafiti za teknolojia bora zinazotumika katika kutoa huduma ya maji na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

### MIUNDOMBINU
Ameboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo kuendelea na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na kuanza kutoa huduma kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Dodoma; kuboresha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, viwanja vya ndege, pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara. Hatua hiyo imechangia kuimarisha huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi.

### AMANI, UMOJA NA MSHIKAMANO
Mafanikio mengine yanajumuisha kuimarika kwa hali ya amani, umoja na mshikamano kupitia jitihada zake ikiwemo utekelezaji wa falsafa yake ya 4R iliyobeba Maridhiano (Reconciliation),Ustahimilivu (Resiliency),Mabadiliko (Reform) na Kujenga upya (Rebuilding).



Rais Samia Suluhu Hassan, ameingia kindaki ndaki kwenye kuutangaza utalii wa Tanzania. Amelifanya hilo kwa yeye mwenyewe kushiriki kwenye kuandaa, kutengeneza na kuzindua filamu ya Royar Tour ambayo wajuzi wa mambo wanasema si jambo rahisi na hata yeye mwenyewe amekiri shuli ilikuwa nzito.






Aidha, ameimarisha ushirikiano wa kimataifa na hivyo kuchangia kuongeza fursa za ajira ndani na nje ya nchi na kuimarisha diplomasia ya uchumi.

**UMUHIMU WA FALSAFA YA 4R**

Utekelezaji wa falsafa ya 4R umesaidia kuongeza wawekezaji nchini; kuimarisha uchumi, demokrasia na ushirikishwaji wananchi kwenye masuala mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**AJIRA MPYA ZAIDI YA MILIONI 7 ZIMAPATIKANA**

Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani, jumla ya ajira 7,015,331 zimezalishwa kupitia sekta ya umma na binafsi.



# *Wananchi watoa kauli*

Kati ya ajira hizo, shughuli za kilimo zimekuwa na mchango mkubwa ambapo zimechangia jumla ya ajira 4,259,771 sawa

na asilimia 60.7 ya ajira zote.
Shughuli nyingine zilizochangia kwa kiwango kikubwa ni biashara za jumla na rejareja asilimia 11.4 na huduma za malazi na chakula asilimia 6.3.

*Kimsingi Rais Dkt. Samia anatosha kuendelea kuwa Rais wa Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na uamuzi wa chama chake wa kumpa nafasi ya kuwa mgombea pekee wa urais kwenye uchaguzi wa Oktoba 2025, unadhihirisha kuwa amefanya kazi kubwa ya kuwaletea maendeleo watanzania kama ambavyo tutaainisha kwenye Makala mbalimbali zilizomo kwenye jarida hili.*

*Rosemary Kimario ambae ni mfanyabiashara wa utalii, anaweka wazi kuwa katika kipindi cha Rais Samia, amefanya biashara zaidi kuliko wakati wowote.*

*Kumbuka dunia ilikumbwa na janga la Korona, hapa wafanyabiashara ya utalii wengi, tulijua tumekwisha, maana hali ilikuwa ni mbaya, lakini mama amekuja kutukomboa, mambo aliyoyafanya kiukweli yametusaidia sana."*

Ramadhani Said Kitundu mkazi wa Mbopo, jijini Dar *es salaam, ameweka wazi kuwa watakaompinga Rais Sami ani wale waliolewa amani.*

*"Hivi unaitoa wapi nguvu ya kumpinga huyu mama, amefanya mambo makubwa mno, hali ya biashara sasa ni nzuri, uwanja wa kisiasa nauona uko hurukwa vyama vyote vinavyofuata sheria, miundombinu inajengwa kila mahali, binafsi naamini anastahili kuendelea kutuongoza."*




Ujenzi wa mji mpya wa kiserikali unaendelea jijini Dodoma na kumekuwa na ongezeko



## VIWANDA NA BIASHARA VYACHANGIA ZAIDI YA TRILIONI 20









## VIWANDA NA BIASHARA VYACHANGIA ZAIDI YA
# TRILIONI 20

NA MWANDISHI WETU

Katika kipindi cha miaka minne ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan madarakani, sekta ya viwanda na biashara imekuwa moja ya nguzo muhimu za ukuaji wa uchumi nchini.

Ikumbukwe kuwa sekta ya viwanda na biashara ni chimbuko la maendeleo nchini kwa ajili ya kuongeza thamani ya malighafi, kutoa ajira kwa wananchi, kuongeza mapato ya nchi, kuingiza fedha za kigeni na kukuza ubunifu, sayansi na teknolojia.

Katika kipindi cha Rais Samia kumepatikana mafanikio mbalimbali ikiwemo sekta hiyo kuchangia zaidi ya trilioni 20 za makusanyo ya kodi,kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 toleo la 2023 ambayo imesaidia kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini, kuhakikisha fursa mbalimbali za biashara zinapatikana na kuwezesha wafanyabiashara kuuza bidhaa na huduma kwenye masoko ndani na nje ya nchi.
Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, Sheria ya Viwango ya mwaka 2009 na Mkakati wa Mauzo ya Nje kwa lengo la kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini imeboreshwa.

Masuala ya biashara katika ngazi ya Tawala za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na kuandaa mwongozo wa majukumu ya utekelezaji katika ngazi hiyo yamegatuliwa.
Ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi umedhibitiwa kwa kukagua jumla ya shehena za bidhaa 140,452 kabla hazijaingizwa nchini.

Mfumo wa kielektroniki wa taarifa za viwanda ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati umeanzishwa.

Thamani ya bidhaa zilizozalishwa viwandani kutoka shilingi trilioni 20.69 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 26.44 mwaka 2024 imeongezwa

Kongani za viwanda ikiwemo kongani ya Kwala Pwani ambapo viwanda viwili vya nguo na vipodozi zimejengwa na kuendelea na ujenzi wa kongani ya kisasa katika eneo la Kikongo Wilaya ya Chalinze Mkoa wa Pwani.

Kiwanda cha kuunganisha na kutengeneza ndege cha kampuni ya Airplanes Africa Limited kilichopo Morogoro kimeanzishwa ambapo ndege tatu za kubeba abiria wawili mpaka wanne zimetengenezwa; na kuanzishwa kwa kiwanda cha Saphirre Float Glass chenye uwezo wa kuzalisha tani 700 za vioo kwa siku na kuajiri jumla ya wafanyakazi 4,869 wameajiriwa.





Serikali kupitia Balozi zilizoko katika nchi mbalimbali duniani imewezesha upatikanaji wa fursa za masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo katika nchi za Malawi, Afrika Kusini, Marekani, Japan, Uswisi, India, Kenya, Uholanzi na Saudia Arabia.

Serikali ya Rais Samia imewezesha uanzishaji wa viwanda vya sekta binafsi kikiwemo kiwanda cha sukari cha Bagamoyo chenye uwezo wa kuzalisha tani 30,000 za sukari kwa mwaka na ajira 1,500 za moja kwa moja na 9,000 zisizo za moja kwa moja;
Biashara na Utoaji wa Leseni za Biashara kupitia mfumo wa kielektroniki wa usajili wa leseni mtandaoni unaotumika kusajili na kutoa leseni za biashara zimesajiliwa.

Mfumo huo, umewezesha kusajili Majina ya Biashara 105,227, Makampuni 55,009, Alama za Biashara na Huduma 13,275 pamoja na kutoa leseni za viwanda 879, leseni za Biashara kundi 'A' 64,582 na Hataza 125.
Mafunzo ya utaalam na ujuzi wa kiufundi katika uzalishaji bidhaa za usindikaji wa vyakula, matunda, ngozi, ufinyanzi na utengenezaji wa sabuni na vipodozi kwa wajasiriamali 76,283 yametolewa.

Katika kuvutia wawekezaji serikali imebainisha na kutatua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara nchini ambapo changamoto 26 zilibainishwa kati ya hizo 21 zilitatuliwa na tano zilizobaki zinaendelea kufanyiwa kazi;
Kumefanyika uwezeshaji wa kupata masoko nje ya nchi ikiwemo kuratibu ushiriki wa Tanzania katika Maonesho ya EXPO 2020 Dubai ambapo hati za makubaliano 36 zenye thamani ya dola za Marekani bilioni 7.49 katika sekta za utalii, miundombinu, uchukuzi, kilimo, nishati na TEHAMA zilisainiwa baina ya Serikali ya Falme za Kiarabu na Serikali ya Tanzania.

Aidha Serikali kupitia Balozi zilizoko katika nchi mbalimbali duniani imewezesha upatikanaji wa fursa za masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo katika nchi za Malawi, Afrika Kusini, Marekani, Japan, Uswisi, India, Kenya, Uholanzi na Saudia Arabia.

Kumekuwa na uwezeshaji wa kuuza aina 10 za mazao kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Mazao hayo ni pamoja na korosho, ufuta, kahawa, alizeti, mahindi, mpunga, dengu na kokoa;
Wadau mbalimbali wamehamasishwa kujenga na kukarabati miundombinu ya kuhifadhia bidhaa ambapo maghala mapya matano yamejengwa katika maeneo ya Nanyamba, Mangaka, Liwale, Ruangwa na Kibiti.

Maghala mawili yamekarabatiwa katika maeneo ya Mvomero na Singida;
Kiwanda darasa cha kubangua korosho kimejengwa katika Wilaya ya Manyoni (Singida), chenye uwezo wa kubangua zaidi ya tani tatu za korosho ghafi kwa siku na kutoa ajira kwa vijana 70.
Serikali imelipa fidia ya shilingi bilioni 15.4 kwa wananchi 1,142 watakaopisha utekelezaji wa mradi unganishi wa makaa ya mawe Mchuchuma na chuma cha Liganga.

Majengo mapya 12 ya viwanda yamejengwa katika mikoa ya Kigoma (5), Simiyu (1), Dodoma (2), Iringa (1), Morogoro (1), Arusha (1) na Mbeya (1) yatakayotumika kwa ajili ya viwanda vidogo.
Shirika la Viwango Tanzania limewezeshwa kupata Tuzo ya Taasisi Bora za Udhibiti Barani Afrika mwaka 2023 iliyotolewa na Taasisi ya Gazeti la Uongozi la Afrika.

Kumefanyika uhamasishaji wa kuanzisha viwanda 12 vya sekta binafsi ambapo viwanda vitatu ni kwa ajili ya uzalishaji wa dawa za binadamu na viwanda tisa ni kwa ajili ya uzalishaji wa vifaa tiba na vitendanishi.
Kubaini jumla ya bunifu 332 za vijana na kuingizwa kwenye Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) na kuzalisha jumla ya ajira 798,871 ambapo wanaume ni 275,182 na wanawake ni 523,689.


# TRA YAVUKA REKODI ZA MAKUSANYO, SASA YAKUSANYA KODI KIRAFIKI

Serikali kupitia Balozi zilizoko katika nchi mbalimbali duniani imewezesha upatikanaji wa fursa za masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo katika nchi za Malawi, Afrika Kusini, Marekani, Japan, Uswisi, India, Kenya, Uholanzi na Saudia Arabia.






TRA YAVUKA REKODI ZA MAKUSANYO, SASA YAKUSANYA KODI KIRAFIKI



Rais Dkt. Samia ameendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikiwemo kuongeza idadi ya walipa kodi hadi kufikia 6,411,919 mwaka 2024, kuboresha mifumo ya kikodi na kufanya marekebisho ya sheria za fedha zilizopunguza na kuondoa baadhi ya tozo kwenye sekta za uzalishaji.
Aidha utendaji Madhubuti wa Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda nao umekuwa chachu ya kuongezeka kwa makusanyo kwa kila mwezi hatua iliyofanikisha utekelezaji wa miradi mingi inayogusa jamii kutekelezwa kwa fedha za ndani.

Takwimu zinaonesha kuwa karika Mwaka wa Fedha 2021/22 makusanyo yalikuwa zaidi ya shilingi 11.92 triioni kwa muda wa Julai 2021–Februari 2022 (miezi 8), ambayo inafanya wastani wazaidi ya shilingi 1.49 triioni kwa mwezi .

Mwaka wa Fedha wa 2023/24 TRA inakadiriwa kukusanya jumla ya takribani shilingi 27.64 triioni mwaka mzima (2023/24) na shilingi 32.26 triioni kwa mwaka wa 2024/25 ikiwa nis awa na kuvuka lengo la kukusanya kiasi cha shilingi 31.05 triioni.

Makusanyo hayo yakichukuliwa kwa wastani wa mwezi ni karibu shilingi 2.69 triioni, hatua hii inaifanya TRA kuwa na mwendelezo mzuri ukusanyaji kodi kila mwezi tangu Rais Dkt. Samia aingie madarakani.

Aidha kumekuwa na ongezeko la makusanyo kwa kipindi cha Julai 2024 – Machi 2025, katika miezi mitatu ya robo ya tatu (Jan–Machi 2025), jumla ya shilingi 7.53 trilioni zilipatikana ikiwa ni wastani wa shilingi 2.49 triioni kwa mwezi .

TRA imefanikiwa kukusanya asilimia 103–104% ya lengo kwa kila mwezi katika mwaka wa fedha wa 2024/25, na kila mwezi walivuka lengo lao kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo .

Hatua hiyo inatajwa kusukumwa na maboresho yaliyofanywa na Serikali ya Rais Dkt. Samia ikiwa ni Pamoja na kuongeza udhibiti na matumizi ya EFDs, Mfumo wa Shtaka za Kodi (ETS), pamoja na mifumo ya kidijitali (TANCIS, IDRAS). Jitihada hizo zimewezesha mwenendo wa ukusanyaji kodi was taha na kuongeza kiwango cha makusanyo ya mapato ya ndani kufikia shilingi trilioni 13.54 kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2024 ikilinganishwa na shilingi trilioni 8.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020.



# TRA YAVUKA REKODI ZA MAKUSANYO, SASA YAKUSANYA KODI KIRAFIKI

Hatua ya Rais Dkt. Samia kuielekeza TRA, kukusanya kodi kirafiki imechangia kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 120.8 kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, tofauti na ilivyokuwa wakati wa Awamu ya Tano, ambapo kiasi cha shilingi trilioni 91 kilikusanywa katika kipindi chote cha miaka mitano.

Wachumi wanaitaja hatua hiyo ya ongezeko la shilingi trilioni 30 za makusanyo linatokana na Serikali ya Rais Dkt. Samia kufanya maboresho kwenye mifumo ya ukusanyaji kodi, kuimarisha matumizi ya kiteknolojia ndani ya TRA, kuwaongezea uelewa walipa na uaminifu kwa serikali na kupambana na mianya ya upotevu wa mapato.
Ongezeko hilo la makusanyo limechangia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuimarisha huduma za jamii.
Mafanikio hayo yamemsukuma Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kuwapongeza Watumishi na Uongozi wa TRA kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa na kufanikiwa kuandika historia mpya ya makusanyo ya Kodi kwa kuvuka malengo kwa miezi 12 mfululizo katika mwaka wa Fedha 2024/2025.

Akifungua kikao cha tathmini ya utendaji kazi wa TRA kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuweka mikakati ya kufanya vizuri kwa mwaka wa fedha 2025/2026 jijini Arusha Julai 08.2025 Waziri Mkuu amesema kazi iliyofanywa na TRA imefanikishwa na lugha moja inayozungumzwa na Watumishi pamoja na uongozi wa TRA ndiyo maana wamekusanya Sh. Trilioni 32.26 sawa na asilimia 103 ya lengo la Sh. Trilioni 31.5.

Waziri Mkuu Majaliwa mesema Serikali inatambua, inaheshimu na inathamini kazi kubwa inayofanywa na TRA na ipo tayari kuiondolea vikwazo vya kisera, kisheria na kikanuni kama vipo ili indelee kufanya vizuri huku akiwafikishia salamu za pongezi kutoka kwa Rais Dkt. Samia.

Waziri Mkuu amesema mafanikio makubwa yanayoonekana yanatoa picha kwamba TRA imeendelea kufanya kazi kwa kujali uzalendo ambayo ndiyo njia sahihi ya kufika kwenye mafanikio.

"Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa TRA kila unapohitajika ili iendelee kufanya vizuri na kusaidia kuhamasisha wananchi kujua umuhimu wa kulipa Kodi" amesema Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu ameiagiza TRA kupitia kitengo chake cha uchunguzi kufuatilia na kuwabaini wageni wote wanaofanya biashara nchini bila kulipa kodi na kuwachukulia hatua huku akiwahimiza watanzania kuendelea kulipa kodi kwa hiari.

"Hakikisheni kila anayestahili kulipa kodi analipa bila kujali utaifa wake, nchi nyingine sheria zao ni kali ukikwepa kodi unachukuliwa kama muhujumu uchumi" alisema Waziri Mkuu.

Kwa upande wake Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu Nchemba ameshauri miradi inayotekelezwa kwa Kodi iwekewe mabango kauli ambayo imeungwa mkono na Waziri Mkuu na kuwaelekeza wakuu wa mikoa kuainisha miradi mikubwa iliyojengwa kwa Kodi kwenye maeneo yao ili iwekewe mabango.






## TRA YAVUKA REKODI ZA MAKUSANYO, SASA YAKUSANYA KODI KIRAFIKI

Dkt. Mwigulu amesema ipo haja ya kuwafanya Watanzania waelewe maendeleo waliyonayo yanatokana na Kodi huku akizitaka Taasisi za Umma na Watumishi wa Umma kuhakikisha wanadai risiti kwa kila manunuzi wanayofanya ili kuchangia nchi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TRA, Mussa Uledi amesema miongozo ambayo imekuwa ikitolewa na Rais Dk. Samia ya kukusanya Kodi katika mazingira rafiki ndiyo imewezesha TRA kuvuka malengo kwa miezi 12 mfululizo na kuwashukuru Walipakodi kwa kuendelea kushirikiana na kuiamini TRA.

Amesema ni matamanio ya Rais kuona Tanzania inajitegemea kibajeti na hatuwezi kufikia malengo hayo kama Kodi isipokusanywa hivyo ni wajibu kwa kila mmoja kuona umuhimu wa kulipa kodi.








Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Juma Mwenda amewashukuru Walipakodi kwa kuiwezesha TRA kuvuka malengo ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kuahidi kuendelea kuwasikiliza na kutatua changamoto zao kwa wakati pamoja na kuendelea kuwezesha biashara nchini.

Amewapongeza Watumishi wa TRA kwa kujituma licha ya kutopendwa na wengi na kuwataka waendelee kuchapa kazi ili kuwezesha kufikiwa kwa lengo jipya la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ambalo ni Sh. Trilioni 36.

Kamishna Mkuu Mwenda amemshukuru Rais Dkt. Samia na Serikali kwa ujumla kwa kuiwezesha TRA kufanya kazi zake kwa Uhuru na kuipa miongozo, vitendea kazi pamoja na nyongeza ya Watumishi.

Kwa upande wake Mkuu wa mkoa wa Arusha, Kenani Kihongosi amewapongeza Watumishi wa TRA kwa kufanya kazi kubwa iliyowezesha kuvuka malengo ya makusanyo na kueleza kuwa fedha hizo zinategemewa kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwemo Maji, Afya, Elimu na Miundombinu.








# VIWANJA 12 VYA NDEGE VYABORESHWA, NDEGE 11 ZIMENUNULIWA

NA MWANDISHI WETU




Miaka minne ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan madarakani imetosha kufanya mageuzi makubwa kwenye eneo la usafiri wa Anga kwa kununua ndege mpya saba, kujenga na kukarabati viwanja vya ndege 11 kama msingi wa Dira 2050.


Viwanja vya ndege vilivyokarabatiwa ni vile vya Rais amejenga Songwe (Mbeya), Mtwara, Songea, Iringa, Geita, Msalato, Kigoma, Tabora, Sumbawanga, Shinyanga, Lake Manyara Tanga na Musoma, huku uwanja wa ndege wa Kimataifa wa msalato ukijengwa.

Kazi nyingine zilizotekelezwa na Rais Dkt.Samia ndani ya miaka minne ni kuendelea kuliimarisha Shirika la Ndege Tanzania - ATCL kwa kununua ndege saba (7) ambapo ndege sita (6) ni za abiria na ndege moja (1) ni ya mizigo hivyo Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 kutoka ndege tisa (9) zilizokuwepo mwaka 2020/21.
Rais Dkt. Samia alisema uamuzi wa kununua ndege ya mizigo unatokana na kukua kwa uchumi wa nchi na kuongezeka kwa wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa zao kutoka na kuingia nchini na hasa wakulima wa mbogamboga na maua.
"Kwa sasa Tanzania inazalisha sana maua na mbogamboga hivyo Ndege ya Mizigo ni muhimu,itawarahisishia wafanyabiashara wa bidhaa hiyo kuyafikia masoko kwa haraka."

Kwa upande wake Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, ameliambia jarida hili kuwa Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege nchini, ikiwepo mradi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, ambacho kipo katika hatua ya juu ya utekelezaji.
"Ujenzi sehemu ya kwanza ikihusisha njia ya kuruka na kutua ndege (runway) na miundombinu mingine imefikia asilimia 87, huku ujenzi wa jengo la abiria, mnara wa kuongozea ndege na miundombinu mingine yote umefikia asilimia 53," alisema Waziri Ulega.

Serikali kupitia Balozi zilizoko katika nchi mbalimbali duniani imewezesha upatikanaji wa fursa za masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo katika nchi za Malawi, Afrika Kusini, Marekani, Japan, Uswisi, India, Kenya, Uholanzi na Saudia Arabia.

# KILOMITA 2,131.26 ZA BARABARA ZA LAMI ZIMEJENGWA








Katika kuhakikisha Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kuleta tija kwa wananchi imeendelea kutekeleza sera ya kuunganisha makao makuu ya mikoa kwa kiwango cha lami. Katika kipindi cha mwaka 2020 – 2024, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:

Kujenga barabara za lami katika barabara kuu za mikoa na wilaya zenye urefu wa kilomita 2,131.26 na kuongeza mtandao wa barabara za lami kutoka kilomita 13, 235.1 mwaka 2020 hadi 15,366.36 mwaka 2024;

Kujenga barabara za changarawe za wilaya zenye urefu wa kilomita 12,876 na kuongeza mtandao wa barabara za changarawe kutoka kilomita 29,183.17 mwaka 2020 hadi 42,059.17 mwaka 2024;

Kuunganisha Mikoa ya Singida-Tabora (Nyahua – Chaya kilomita 85.4) na Tabora – Katavi (Tabora - Ipole – Koga – Mpanda kilomita 386) kwa barabara za lami. Aidha, kazi ya kuunganisha makao makuu ya mikoa ya Katavi na Kigoma, Kigoma na Tabora, Singida na Mbeya, Singida na Simiyu, Arusha na Manyara, Arusha na Simiyu, Morogoro na Ruvuma, Kigoma na Kagera kwa kiwango cha lami inaendelea;

Kukamilika kwa ujenzi wa madaraja makubwa ya Kitengule (Kagera), Wami (Pwani), Msingi (Singida), Tanzanite (Dar es Salaam), Kiyegeya (Morogoro), Berega (Kilosa), Gerezani (Dar es Salaam), Mpwapwa (Dodoma) na Ruhuhu (Ruvuma). Vilevile, ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) umefikia asilimia 94.4;

Kukamilika kwa ujenzi wa barabara za: Kiluvya – Mpiji; Itoni – Ludewa – Manda, sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50); Njombe - Makete - Isyonje, sehemu ya Moronga – Makete (km 53.5); Nyamuswa – Bunda – Kisorya, sehemu ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4); na Loliondo – Mto wa Mbu, sehemu ya Waso – Sale (km 50); na njia nane ya Kimara – Kibaha (km 19.2);

Kuanzisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kukusanya mapato katika hifadhi za barabara zilizo chini ya TARURA. Aidha, ujenzi wa Mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato kutoka katika hifadhi za barabara za kitaifa ambazo husimamiwa na TANROADS upo katika hatua za ukamilishaji;




> "Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake amekuwa akihimiza uhifadhi wa mazingira na kushughulikia changamoto zinazosababishwa na matukio ya hali ya hewa



NSSF
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

MIFUMO YA HUDUMA BINAFSI KWA **MWANACHAMA NA MWAJIRI**

Mifumo hii ni ya mwajiri **"Employer Portal"** na mwanachama **"Member Portal"** inapatikana kupitia tovuti ya Mfuko **"www.nssf.or.tz"** bofya kifute cha **"Self Service"** (Huduma Binafsi).




- Mfumo wa **"Employer Portal"** ni maalum unaowawezesha waajiri kuangalia michango ya wafanyakazi wao, unaohamasisha uwazi na uwajibikaji kati ya Mfuko na mwajiri.
- Mfumo wa **"Member Portal"** unamuwezesha mwanachama kupata taarifa za michango yake.

@NssfTanzania

## MAKUSANYO YAONGEZEKA

# BANDARINI

**AJIRA ZAIDI YA 161,000 ZAZALISHWA**



NA MWANDISHI WETU

Moja ya maeneo ambayo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekabiliana nayo kishujaa ni uwekezaji kwenye eneo la Bandari, hasa Bandari ya Dar es Salaam, ambalo sasa limekuwa sehemu ya maeneo tegemezi ya makusanyo ya mapato nchini, Pamoja na kuongeza ajira.

Ukosoaji ulikuwa ni mkubwa wakati wa kutoka kwa baadhi ya watu wakiwemo wanasiasa na viongozi wa dini, ambao walikuwa wakiupinga kabisa ujio wa kampuni ya DP WORLD.

Pamoja na ukosoaji huo Rais Dkt. Samia hakuyumba na badala yake alisimamia kile alichoamini ni sahihi, hatua iliyoungwa mkono na wananchi wengi na hatimae sasa hali imebadilika kabisa ndani ya bandari ya Dar es Salaam.

Katika kipindi kifupi cha mwaka 2024 mara baada ya ujio wa DP World kulikuwa na mafanikio makubwa ambapo kasi ya upakuaji na usafirishaji mizigo iliongezeka kutoka tani 141,889 hadi kufikia tani 168,336 akiwa ni ongezeko la zaidi ya asimia 18, mud awa kupakua mizigo umetoka kuwa siku saba hadi siku tatu kwa meli kubwa.

Meli sasa hazisubiri kwa muda mrefu, badala yake zinasubiri kwa siku saba tu kuingia kwenye eneo la upakiaji au ushushaji wa mizigo.

Makusanyo yameongezeka kutoka shilingi bilioni 850 hadi zaidi ya trilioni moja na kiasi kikubwa cha fedha za uendeshaji wa shughuli za bandari zimepungua kutoka asilimia 15.1 hadi asilimia 2.7 na hii ni kwa mujibu wa taarifa kutoka mamlaka ya Bandari Tanzania.

Kimsingi uwepo wa DP World -Dar es Salaam umekuwa na matokeo chanya ambapo pamoja na mambo mengine kumekuwa na uwekezaji wa mashine za kisasa, mifumo ya ICT imara (TANCIS na TeSWS), na huduma bora imeongeza uaminifu wa bandari kwa wateja wa kimataifa.

Aidha katika kipindi cha miaka minne ya Rais Dkt. Samia kumefanyika maboresho ya miundombinu ya Bandari ikiwemo uboreshaji wa gati Na. 1 – 7, kuchimba kina cha maji kutoka mita 11 hadi mita 14.5 na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli, ujenzi wa gati maalumu (RoRo berth) la kuhudumia meli za magari na eneo la kuegesha magari katika bandari ya Dar es Saalam;
Kukamilisha uboreshaji wa bandari ya Tanga katika awamu ya pili ambapo ukarabati wa gati namba 1 na 2 yenye urefu wa mita 300, ununuzi wa mitambo na kuongeza kina kutoka mita 3 hadi 13 ulikamilika;

Kuongezeka kwa shehena za mizigo bandarini kutoka tani milioni 17.1 mwaka 2020 hadi kufikia tani milioni 28.75 Desemba 2024. Vilevile, idadi ya meli zilizohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara imeongezeka kutoka meli 1,547 mwaka 2020 hadi meli 4,487 mwaka 2024;
Kukamilisha ununuzi wa ndege mbili za injini moja kwa ajili ya mafunzo ya urubani yanayotarajiwa kutolewa katika Chuo Cha Taifa cha Usafirishaji hivyo kuweka historia ya kuanza kutoa mafunzo ya urubani nchini kwa mara ya kwanza;

Kukamilisha ununuzi wa mtambo maalum wa kufundishia kwa vitendo umenunuliwa na kufungwa katika Chuo cha Bahari (DMI) na tayari mtambo huo umeanza kutumika kutoa mafunzo kwa vitendo ya kuhudumia mizigo kwenye meli na vyombo vingine vya usafiri majini;
Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu ambao umefikia asilimia 96 na kukamilisha ukarabati wa meli ya MV Umoja (Wagon Ferry) katika Ziwa Victoria na meli hiyo imeanza kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kati ya bandari ya Mwanza (Tanzania) na bandari ya Jinja (Uganda); na
Kuzalisha jumla ya ajira 161,147 ambapo wanaume ni 150,098 na wanawake ni 11,049.



# HUDUMA ZA JAMII
## ZIMEBORESHWA

Katika upande wa afya kumekuwa na utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo na Mipango mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa inayolenga kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya nchini.

Kutokana na hatua hizo, mafanikio mbalimbali yameendelea kupatikana kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika ili kuimarisha utolewaji wa huduma za afya nchini kwa lengo la kuwezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi.
Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Katika sekta ya afya, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi na ugunduzi; kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya; kuongezeka kwa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi; na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya.

Mafanikio hayo yamesaidia kupunguza idadi ya vifo vya wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano na kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini.

Mafanikio hayo ni pamoja na:
Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Kutolea Huduma ya Afya

i. Kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika maeneo mbalimbali nchini kwa kuongeza vituo kutoka 8,458 mwaka 2020 hadi 9,826 mwaka 2024 sawa na ongezeko la vituo 1,368;

ii. Kuongezeka kwa idadi ya Hospitali zinazotoa huduma ya magonjwa ya dharura (EMD) kutoka saba mwaka 2020 hadi kufikia 116 mwaka 2024;

iii. Kujenga vituo vipya 183 vya kutolea huduma za afya vyenye uwezo wa kutoa huduma za dharura za uzazi ikiwemo upasuaji. Ujenzi uliofanyika umeongeza vituo hivyo kutoka 340 mwaka 2020 hadi 523 mwaka 2024 kwa mikoa yote nchini;

iv. Kujenga majengo ya kuwatunza watoto waliozaliwa na changamoto za afya (NICU) katika hospitali 66 kwenye mikoa 24 na kukarabati majengo 39 kwenye Mikoa 15 ya Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Geita, Kigoma, Katavi, Lindi, Mtwara, Manyara, Arusha, Tanga, Dodoma, Morogoro, Mwanza.

Jitihada hizo zimeongeza mahudhurio manne ya kliniki ya mama wajawazito kutoka asilimia 85 mwaka 2021 hadi asilimia 116 mwaka 2024;

v. Kukamilisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa nne katika mikoa ya Songwe, Geita, Katavi na Simiyu ambapo kwa sasa zinaendelea kutoa huduma kwa wananchi;

vi. Kukamilisha ujenzi wa hospitali mpya 50 za Halmashauri za Wilaya na kukarabati hospitali 48 za Halmashauri za Wilaya ambapo hospitali zote zinaendelea kutoa huduma kwa wananchi;

vii. Kukamilisha ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda za Chato, Mtwara, Hospitali ya Kanda ya Kusini na Hospitali ya Uhuru Chamwino Mkoani Dodoma ambazo zimeanza kutoa huduma; na


viii. Kuongeza idadi ya vitanda vya kulaza wagonjwa hadi kufikia vitanda 126,209. Huu ni uwekezaji mkubwa kwani, kwa mujibu wa viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO), kila watu 1,000 uwiano ni vitanda 2.5, hivyo Tanzania imefikia uwiano wa 2.1 kwa kila watu 1,000.



Katika sekta ya afya, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi na ugunduzi; kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa na bidhaa za afya; kuongezeka kwa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi; na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya.

# MAWASILIANO YAGUSA

## MAISHA YA WENGI



> Kuongeza idadi ya watumiaji wa mtandao wa intaneti kutoka asilimia 43 ya 2G mwaka 2020 hadi asilimia 89 kwa 3G na asilimia 84 kwa 4G kwa mwaka 2024 pamoja na kuanza kwa huduma za 5G na fiber mlangoni

Serikali imeimarisha sekta ya mawasiliano kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupokea au kutoa habari kuhusu masuala mbalimbali yakiwemo ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2024 mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa wigo wa mawasiliano ya kasi ya (broadband) kutoka asilimia 45 mwaka 2020 hadi asilimia 63 mwaka 2024. Ongezeko hili limetokana na ujenzi wa kilomita 4,442 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi wa minara 758 ya simu na kuongeza nguvu uwezo wa minara ya simu kutoka teknolojia ya 2G kwenda 3G,4G na 5G;

ii. Kuongeza idadi ya watumiaji wa mtandao wa intaneti kutoka asilimia 43 ya 2G mwaka 2020 hadi asilimia 89 kwa 3G na asilimia 84 kwa 4G kwa mwaka 2024 pamoja na kuanza kwa huduma za 5G na fiber mlangoni;

iii. Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu za viganjani nchini kutoka asilimia 95 mwaka 2020 na kufikia asilimia 97 mwaka 2024;

iv. Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya intaneti ya kasi katika maeneo ya umma kutoka asilimia 23 mwaka 2020 hadi asilimia 57 mwaka 2024;
v. Kiwango cha uunganishaji wa taasisi za Serikali na miundombinu ya mtandao wa kasi kimefikia asilimia 50 mwaka 2024 kutoka asilimia 20 mwaka 2020;

vi. Kuwezesha ujenzi wa kiwanda kimoja cha kutengeneza nyaya za mkongo wa mawasiliano (optic fiber) kilichopo Mkuranga Pwani;



vii. Kuweka anwani za makazi 12,840,805 katika kaya 12,030,000, kusimika nguzo 229,417 za majina ya barabara na kubandika vibao vya namba za anwani 7,439,715 na wananchi 9,299 wanatumia programu ya NaPA;

viii. Kuimarisha mazingira ya ushindani kwa watoa huduma yaliyochangia kupungua kwa gharama za rejareja za kupiga simu kutoka wastani wa shilingi 72 kwa dakika ndani ya mtandao mmoja na wastani wa shilingi 75 nje ya mtandao mmoja mwezi Oktoba, 2020 kufikia shilingi 26 kwa dakika ndani ya mtandao mmoja na Shilingi 28 kwa dakika nje ya mtandao mmoja mwezi Desemba, 2024 mtawalia. Aidha, gharama za ujumbe wa maneno zimepungua kutoka wastani wa shilingi 23 mwezi Oktoba, 2020 hadi wastani wa shilingi 7.8 mwezi Desemba, 2024;

ix. Kuimarisha usiri na faragha wa taarifa binafsi za wananchi kitaifa na kimataifa kwa kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi mwaka 2022 sambamba na kuunda Tume mahususi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sheria; na Kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo ya mtambo wa TTMS kutoka shilingi bilioni 9.03 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 66.88 mwaka 2024.















# UTAWALA BORA UKO KATIKA MIKONO SALAMA

Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya utu, haki, ushirikishwaji, demokrasia, uwajibikaji, uwazi na usawa kwa wote. Utekelezaji uliofanyika katika kipindi cha miaka minne




# UTAWALA BORA UKO KATIKA MIKONO SALAMA

Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya utu, haki, ushirikishwaji, demokrasia, uwajibikaji, uwazi na usawa kwa wote. Utekelezaji uliofanyika katika kipindi cha miaka minne ni kama ifuatavyo:

i. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ilipokea malalamiko 3,243. Kati ya hayo, malalamiko 2,480 yalihitimishwa na malalamiko 763 yanaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Aidha, jumla ya klabu 306 za Haki za Binadamu zilianzishwa katika shule 100 na vyuo 25;

ii. Jumla ya wananchi 467,326 walifikiwa na elimu kwa umma kuhusu katiba na uraia ambapo wadau wa elimu waliainisha masula ya kikatiba yanayohitajika kujumuishwa kwenye mitaala ya elimu;

iii. Kutoa mafunzo ya maadili ya viongozi na udhibiti wa mgongano wa maslahi kwa wadau 68,570;

iv. Kuwezesha TAKUKURU kufanya operesheni mbalimbali zilizookoa jumla ya shilingi bilioni 51.65; na

v. Kutoa msaada wa kisheria kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia iliyofanyika katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Shinyanga, Ruvuma, Simiyu, Singida na Njombe pamoja na maadhimisho ya kitaifa ikiwemo sabasaba na nanenane ambapo jumla ya wananchi 734,904 ikiwemo wanawake 243,043, watoto 239,352 na wanaume 252,509 walifikiwa.

**SERIKALI ZA MITAA NI SHWARI**

Serikali imeimarisha na kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria; kuratibu shughuli za utoaji wa huduma mijini na vijijini kama vile usafiri, usafirishaji na usafi wa mazingira; kusimamia shughuli za elimu msingi na sekondari; kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji wa huduma za afya ya msingi, ustawi wa jamii na lishe; na kuratibu shughuli za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo.

*Kupitia mikakati hiyo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo:*

i. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato katika halmashauri kwa kuanzisha mfumo wa TAUSI pamoja na kununua mashine za kukusanyia mapato (POS) 6,773. Jitihada hizo zimeongezeka makusanyo ya mapato ya ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoka shilingi trilioni 2.91 mwaka 2020 na kufikia shilingi trilioni 3.82 mwaka 2024;

ii. Kuajiri maafisa ugani 807 ambao wamesambazwa katika vijiji mbalimbali nchini na kufanya vijiji 7,391 kuwa na maafisa ugani wanaotoa huduma za ugani katika vijiji hivyo;

iii. Kuongeza urefu wa barabara za majiji na miji zilizowekewa taa za barabarani kutoka kilomita 56 mwaka 2020 hadi kilomita 125 mwaka 2024; na

iv. Kuimarisha utoaji wa huduma ya Mabasi yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu na ya Nne ya miundombinu ya barabara ya mwendokasi na kuanza kutoa huduma kwenye awamu ya pili kwa njia ya Mbagala Jijini Dar es Salaam.

**MAFANIKIO LUKUKI UCHAGUZI SERIKALI ZA MITAA 2024**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliendesha kwa mafanikio makubwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba, 2024.



Q&A

NA JIMMY KIANGO

# AG:Ni muhimu kuujua utawala wa sheria

Serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kuzingatia misingi ya utu, haki, ushirikishwaji, demokrasia, uwajibikaji, uwazi na usawa kwa wote. Utekelezaji uliofanyika katika kipindi cha miaka minne

Moja ya maeneo yanayobeba maisha ya watu ya kila siku ni eneo la utawala wa sheria na dhana ya haki na wajibu wa serikali na watu wake.
Ugumu wa eneo hili unasukumwa na kukosekana kwa ufafanuzi wa kina na elimu ya kutosha kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuishi kwa kufuata sheria.

Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili, jarida la tz&beyond, lilimtafuta Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari ili kulitolea ufafanuzi na elimu ya kutosha kwa jamii, lengo likiwa ni kuepusha upotoshaji unaofanywa na baadhi ya wanasiasa juu ya kukosekana kwa utawala wa sheria. Fuatilia mahojiano haya:

**TZ&BEYOND:** Nini tafsiri ya haki na wajibu kwa maisha ya kawaida ya kila Mtanzania?
**AG:** Haki ni ni stahili halali ya mtu kupata, kufanya au kufurahia jambo fulani kwa mujibu wa sheria, utu na misingi ya kijamii. Wajibu ni jukumu au uaminifu wa mtu kutimiza matakwa ya jamii, sheria na maadili ya taifa.

Kwa mantiki ya kimataifa: Ibara ya 29(1) ya Azimio la Haki za Binadamu (UDHR, 1948) linabainisha kwamba:
"Kila mtu anao wajibu kwa jamii anamoishi, ambayo pekee ndiyo inayowezesha ukuaji huru na kamili wa utu wake"
Maana yake haki haiwezi kutekelezwa nje ya mfumo wa kijamii unaohitaji pia uwajibikaji. Ibara ya 27(1) ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (African Charter on Human and Peoples' Rights (1981) inaeleza kuwa:
"Kila mtu anao wajibu kwa familia, jamii na jumuiya ya taifa lake..."

Maana yake, katika maisha ya kawaida, haki na wajibu ni mfumo wa uhusiano wa kijamii unaotegemeana; kwamba haki huanzisha matarajio, lakini wajibu huweka uhusiano wa kijamii unaowezesha utekelezaji wake.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo mfumo mkuu wa sheria nchini unaobainisha misingi ya haki na wajibu, ambao utekelezaji wake unategemea sheria, kanuni na taratibu mbalimbali ambazo Nchi hujiwekea ili kukidhi misingi iliyobainishwa na Katiba.
Kwa mfano:

Ibara ya 14 ya Katiba inatamka kuwa, mtu ana haki ya kuishi; haki hiyo inaenda sambamba na wajibu wa kuheshimu uhai wa mtu mwingine kwa kuepuka vitendo vya uvunjifu wa amani na vurugu vinavyoweza kuhatarisha uhai wa mtu mwingine na kusababisha kifo kinyumbe na Vifungu vya 196 (Mauaji) na 211 (Jaribio la Mauaji) vya Kanuni za Adhabu, Sura 16.





Mtanzania ana haki ya kupata huduma za afya, lakini ana wajibu wa kulinda afya ya wengine, kwa mfano kutii miongozo ya afya ya jamii kama vile chanjo na tahadhari za mlipuko wa magonjwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 206 (Wajibu wa Mtu kwa Mtu Mwingine) cha Kanuni za Adhabu, Sura ya 16.

**TZ&BEYOND:** Haki zinazosemwa katika Katiba ni zipi na wajibu ni upi?

**AG:** Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inaorodhesha haki katika ibara kuanzia ya 12 hadi 29, zikiwemo:

1. (i) Haki ya uhai, Ibara ya 14,
2. (ii) Haki ya usawa mbele ya sheria, Ibara ya 13,
3. (iii) Haki ya uhuru wa mtu binafsi, Ibara ya15,
4. (iv) Haki ya faragha, Ibara ya 16,
5. (v) Haki ya kutoa maoni, Ibara ya 18,
6. (vi) Haki ya kushiriki katika siasa, Ibara ya 21,

7. (vii) Haki ya kumiliki mali, Ibara ya 24

Wajibu:

Ibara ya 25(1) inaeleza:

"Kila mtu ana wajibu wa kushiriki kikamilifu katika kazi halali na shughuli za maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla"

Wajibu unaojitokeza kwa mujibu wa Katiba unahusisha;

1. (i) Kutii sheria, Ibara ya 26
2. (ii) Kulinda mali ya umma, Ibara ya 27
3. (iii) Ulinzi wa taifa, Ibara ya 28
4. (iv) Kuheshimu haki za wengine, Ibara ya 29(5)

**TZ&BEYOND:** Naomba maelezo yako na mifano hai ili wananchi waweze kufahamu hakuna haki isiyokuwa na wajibu.

**AG:** Haki ya kupiga kura

Ibara ya 5 ya Katiba inasema kuwa haki ya kupiga kura ipo kwa kila mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na zaidi. Ibara hii inatekelezwa na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024, kifungu cha 9. Lakini ni wajibu wa mtanzania kujiandikisha kwa hiari, kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa katika Sheria ili aweze kutumia haki hiyo ya kupiga kura.

Maana yake, haki ya kidemokrasia haitekelezeki kama wananchi hawatimizi wajibu wao kisiasa na kiraia.

Haki ya kumiliki mali

Ibara ya 24 ya Katiba, inatambua haki ya kumiliki mali. Aidha, Sheria ya Ardhi, Sura ya 113, inaweka utaratibu wa mtu yeyote kumiliki mali na kumtaka mmiliki kutumia ardhi kwa matumizi sahihi, bila kusababisha madhara ya mazingira au migogoro katika kijamii.

Maana yake ili mtu aweze kutumia haki yake ya kikatiba ya kumiliki mali, anawajibika kuzingatia sheria ili kupata umiliki na kutumia mali hiyo bila kuathiri haki za watu wengine.

Haki ya kujieleza

Ibara ya 18 ya Katiba inatambua haki ya kujieleza au kutoa maoni. Hata hivyo haki hiyo haipaswi kuingilia au kuathiri faragha ya mtu mwingine. Ili kuhakikisha hilo, Sheria mbalimbali zimewekwa ili kuhakikisha haki ya kujieleza inatumika bila athari kwa wengine. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sura ya 443 na Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na matukio kadhaa ambapo baadhi ya watu na makundi ya watu wamekuwa wakitumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kusambaza taarifa za uwongo na kuchochea chuki au kuingilia faragha za wengine.

Mfano katika shauri la Benard Camillius Membe dhidi ya Cyprian Musiba na wengine ambapo Mahakama ilibainisha kuwa uhuru wa kutoa maoni hauhusishi kutoa tuhuma za uwongo au matusi dhidi ya viongozi wa umma bila ushahidi.

(iv) Haki ya kufanya mikutano au maandamano ya amani. Ibara ya 20 ya Katiba inatoa haki kwa mtu yeyote kukutana, kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine. Haki hii inaambatana na wajibu wa kuhakikisha kuwa hakuna uvunjifu wa amani.

Aidha, zipo sheria mbalimbali ambazo zimetungwa ili kusimamia haki hii ambapo baadhi ya taratibu zilizowekwa zinajumuisha kupata kibali cha kufanya mikutano.

**TZ&BEYOND:** Utawala wa sheria unaweka vyombo vikuu vitatu katika mizania moja. Serikali, Bunge na Mahakama, hakuna chombo kilicho juu ya mwenzake, bali kila kimoja hutekeleza wajibu wake wa kipekee na ndio hujitofautisha. Kwa muktadha huo, naomba elezea kazi za kila chombo kwa azma ya utawala wa sheria unavofanya kazi bila kuleta mgongano.

**AG:** Ni kweli kwamba, Utawala wa sheria umeweka vyombo vikuu vitatu katika mizania moja na hakuna chombo kilicho juu ya kingine.

Kwa mujibu wa ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mamlaka yametolewa kwa vyombo vitatu yaani Serikali imepewa jukumu la kusimamia utendaji, Bunge limepewa kazi ya kutunga Sheria na Mahakama imepewa majukumu ya kutafsiri sheria.





# MAMBOYA NJE NGUZO YA MAENDELEO

Mwelekeo wa sasa wa Tanzania juu ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa unatilia mkazo katika masuala ya kuimarisha amani, uhuru, maslahi ya Taifa, na diplomasia ya uchumi bila kuathiri misingi ya sera, mila na desturi zetu.

Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali imeendelea kushiriki katika majadiliano ya kimataifa na jumuiya za kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama husussan Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;

kuendelea kuratibu na kutekeleza diplomasia ya uchumi ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya mpango wa kitaifa wa utekelezaji wa diplomasia ya uchumi; kuboresha Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001 Toleo la mwaka 2024; pamoja na kuratibu ziara za kikazi za viongozi wakuu wa Kitaifa nje ya nchi na ziara za viongozi wakuu wa mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa hapa nchini kwa lengo la kudumisha uhusiano wa kidiplomasia na kutumia fursa za kiuchumi.

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ni kama ifuatavyo:

i. Kuratibu mikutano 25 ya ubia wa maendeleo baina ya Tanzania na nchi za Afrika, Ulaya, Amerika, Asia, Australia na Mashariki ya Kati;

ii. Kujenga mahusiano ya kidiplomasia na kiuchumi ambapo;

a) Kwa upande wa kiuchumi, ziara ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchini Jamhuri ya Korea, ilifanikisha kupatikana fedha zenye masharti nafuu kiasi cha Dola za kimarekani bilioni 2.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi katika sekta za maendeleo.

Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kujenga kituo cha kisasa cha mafunzo ya reli, chuo cha mafunzo ya anga na urubani, kituo cha kusambaza umeme Nyakanazi, kituo cha uchenjuaji wa madini na maabara za kisasa za vito, Kongani ya Viwanda Bagamoyo, Bandari ya Wete, Bandari ya Uvuvi Bagamoyo, Barabara za Zanzibar, Ukumbi wa Mikutano Zanzibar, Studio ya Filamu ya Kisasa na Kituo cha burudani mbalimbali kwa ajili ya ajira za vijana; Uendelezaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, na Ununuzi wa Mabehewa ya Abiria na Mizigo kwa ajili ya Kipande cha Reli kutoka Mwanza hadi Isaka.

Pia, ulisainiwa Mkataba wa masharti nafuu wenye kiasi cha Dola za Marekani milioni 163.6 kwa ajili ya kugharamia mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Binguni na Kituo cha Mafunzo ya Afya Zanzibar;

b) Kwa upande wa Diplomasia, mwaka 2024 Tanzania ilizidi kuimarika na kutuletea manufaa makubwa katika nyanja za kimataifa ambapo tulipata heshima ya kushiriki Mkutano wa G20.

Mkutano huo uliazimia kuunga mkono jitihada za upatikanaji wa nishati safi na kuimarisha uwekezaji kwenye kilimo ili kuondosha njaa na umaskini duniani.

Aidha, Tanzania ilishinda nafasi ya kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika; na

c) Aidha, Serikali ya Watu wa China China, ilifungua milango ya soko la bidhaa mbalimbali ikiwemo mihogo mikavu, soya, mabondo ya samaki, mazao ya baharini, asali, mashudu ya alizeti na pilipili. Pia, Tanzania, China na Zambia zilikubaliana kuifufua reli ya TAZARA ili kuboresha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo;

d) Kwa upande wa ukanda wa SADC, Tanzania ilipata heshima ya kupokea Uenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, yenye jukumu la kusimamia masuala ya Ulinzi na Usalama katika Kanda hiyo.




Rais Samia, Kupandisha vyeo watumishi 429,458; kubadilisha kada watumishi 39,600; kuteua watumishi 2,693 katika nafasi mbalimbali



# MASLAHI YA WAFANYAKAZI YAMEBORESHWA

Uwepo wa nguvu kazi yenye weledi, maarifa, ujuzi na uzoefu ni nguzo muhimu kwa maendeleo endelevu ya nchi kutokana na ufanisi utekelezaji wa shughuli za kila siku. Hivyo, ni muhimu kuwekeza katika kujenga na kuendeleza nguvu kazi kwa kutoa mafunzo, elimu bora na uzoefu kwa vitendo ndani na nje ya nchi.
Katika kipindi cha miaka minne, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira ya utendaji kazi ambapo mafanikio yafuatayo yalipatikana:

i. Kuboresha maslahi ya wafanyakazi kwa kuongeza viwango vya posho za kujikimu kwa safari za kikazi ndani ya nchi, posho ya kazi za masaa ya ziada, kupunguza kodi ya mapato (PAYEE), kuongeza kima cha chini cha mshahara kinachopaswa kukatwa kodi kutoka shilingi 170,000 hadi 270,000; kuboresha umri wa watoto wategemezi wa mwanachama wa NHIF kutoka miaka 18 hadi miaka 21; kufuta tozo (retention fee) ya asilimia 6 iliyokuwa ikitozwa katika mishahara ya watumishi wa umma walionufaika na mikopo ya elimu ya juu. Kwa kufanya hivyo, serikali ilisamehe takribani shilingi bilioni 14.78 kutoka kwa watumishi wa umma;

ii. Kuongeza mshahara kwa watumishi wa umma kwa asilimia 23.3 kwa kima cha chini cha mshahara pamoja na kutoa nyongeza ya mwaka ya mshahara (Annual Increment) kwa mwaka 2023/2024 na 2024/2025;

iii. Kupandisha vyeo watumishi 429,458; kubadilisha kada watumishi 39,600; kuteua watumishi 2,693 katika nafasi mbalimbali za uongozi; kusafisha taarifa za kiutumishi za watumishi 141,574; kubadilisha vyeo vya watumishi 9,399; kurekebisha majina ya watumishi 1,941; kufanya mabadiliko ya mshahara binafsi kwa watumishi 8,424; kurejeshwa kwenye utumishi wa umma watumishi 2,022; na kuajiri watumishi 102,154 katika taasisi za umma;

iv. Kulipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wastaafu 9,651 kutoka kwa waajiri yenye thamani ya shilingi bilioni 32.66 pamoja na madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 130,463 yenye thamani ya shilingi bilioni 226,584;

v. Kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma 571,586 kuhusu matumizi na utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi

**...Kalipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wastaafu 9,651**



# KERO ZA MUUNGANO NYINGI ZIMETATULIWA

Maadhimisho hayo ni alama ya kudumisha utaifa wetu uliojengwa katika misingi imara ya Muungano wa jamii mbili zenye udugu wa asili. Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji, mafanikio yafuatayo yamepatikana:

Muungano ni nguzo ya umoja, mshikamano, amani na utulivu wa wananchi wa pande zote za muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar.

Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuulinda, kuuthamini na kuudumisha muungano ili kuwawezesha wananchi kufurahia matunda yake kwa kuhakikisha Muungano wetu unaimarishwa, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yanalindwa pamoja na kuwepo kwa umoja, mshikamano na utulivu.

Aidha, mwaka 2024 nchi iliadhimisha kwa mafanikio makubwa miaka 60 ya Muungano pamoja na miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Maadhimisho hayo ni alama ya kudumisha utaifa wetu uliojengwa katika misingi imara ya Muungano wa jamii mbili zenye udugu wa asili. Katika kipindi cha miaka minne ya utekelezaji, mafanikio yafuatayo yamepatikana:

i. Kuimarisha ushirikiano wa Wizara/ Idara na Taasisi zisizo za muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika mambo yasiyo ya muungano. Katika kutekeleza suala hilo, Serikali imeratibu vikao 60 vya ushirikiano baina ya sekta zisizo za muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

ii. Kuimarisha uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ vya kushughulikia masuala ya muungano kwa lengo la kutatua changamoto kwa kasi zaidi ambapo hoja 15 zimezipatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano.

Hoja hizo ni pamoja na:

a) Uvuvi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu;

b) Uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar katika soko la Tanzania Bara;

c) Ajira kwa watumishi wa Zanzibar katika taasisi za muungano;

d) Mgawanyo wa mapato yatokanayo na misaada ya kibajeti;

e) Mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja;

f) Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba;

g) Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri;

h) Usimamizi wa ukokotoaji na ukusanyaji wa kodi kwenye huduma za simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar;

i) Mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar;

j) Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Rufaa la Kodi (TRAT) kutoka Zanzibar;

k) Uteuzi wa mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana kutoka Zanzibar;

l) Malalamiko ya wafanyabiashara wa Zanzibar kutozwa kodi mara mbili;

m) Kodi ya Mapato (Pay as You Earn – PAYE) na kodi ya zuio (Withholding Tax);

n)Ongezeko la gharama za umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwenda Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO); na Mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ujenzi wa kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume (Terminal III).



# DKT. NCHIMBI CHADEMA WASILAZIMISHWE KUSHIRIKI UCHAGUZI 2025

Mgombea Mwenza wa Urais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amewataka Watanzania wasiwalazimishe viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kushiriki Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 29,mwaka huu wa 2025.

Dkt. Nchimbi alitoa kauli hiyo kutokana na msimamo wa viongozi wa Chadema kuwa kamwe hawatashiriki uchaguzi huo hadi pale kutakapofanyika mabadiliko ya Katiba wakibeba kauli mbiu ya 'No Reform, No Election'.

Viongozi wa Chadema wamekuwa wakiwahamasisha Watanzania wasishiriki uchaguzi kwa madai kuwa Sheria na Kanuni za sasa hazitoa fursa sawa kwa vyama vyote vya siasa. Akiwa Songea, mkoani Ruvuma, mwanzoni mwa mwaka huu, Dkt. Nchimbi ambae pia alikuwa Katibu Mkuu wa CCM, alisema hakuna sababu ya kuwasaka wapinzani hao kwa kuwa wana uhuru na haki ya kususia au kushiriki uchaguzi.

Amesema nchi yetu ina utaratibu wa kufanya uchaguzi kila baada ya miaka mitano hivyo Watanzania wasiwe na wasiwasi wa kutokuwepo kwa uchaguzi mwaka huu.

"Hakuna raia anaeweza kusema kuwa uchaguzi hautafanyika kwa kuwa hili ni takwa la kikatiba. Uchaguzi wa mwaka 2025 utafanyika kama ulivyopangwa,"alisema.

Amesema hata Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hana uwezo wa kuzuia uchaguzi usifanyike kwa kuwa hilo ni takwa la kikatiba ambayo ameapa kalinda na kuitetea. "Pamoja na haki ya raia kugombea pia hakuna haki ya kulazimisha chama chochote cha siasa kisiingie kwenye uchaguzi.



TIPER
TANZANIA INTERNATIONAL PETROLEUM RESERVES L.T.D



"KEY FACILITATOR OF PETROLEUM BUSINESS IN THE REGION"





**TIPER** the joint venture company between the government of Tanzania and Oryx Energies SA (OESA) based in Geneva with equal shares 50% each operates the largest storage facility for petroleum in the country. Current storage capacity is 253.7 million litres.

TIPER which used to be known as Tanzanian Italian Petroleum Refining (TIPER) Company Limited, commissioned refinery business in 1966. In year 2000, the refinery business ceased. In 1999 Agippetrol International (BV) - "Agip" sold its assets in TIPER as well as the 50% shareholding of the company to Oryx Energies SA., GENEVA (OESA). The remaining 50% shares continued to be owned by the Government of Tanzania.

Following the liberalization of the downstream petroleum subsector in Tanzania, TIPER found it uneconomical to operate as a refinery. In mid-2000, the company changed its main objective from refining to petroleum product storage. The refinery was decommissioned, scrapped and the plant was then converted in to a refined petroleum storage terminal, whose core business is the bulk storage and handling of refined petroleum products with delivery of the customer's product through cross pumping to other terminals, back-loading for onward transshipment and truck loading for onward sale at local commercial and retail outlets as well as for transit.






**TIPER** operating as a bulk liquid storage entity, stores low sulphur diesel (AGO), Premium Motor Spirit " (PMS), Dual Purpose Kerosene (DPK) and Heavy Fuel Oil (HFO 180) which is widely used in industrial applications. TIPER operating as storage facility has facilitated to a greater extent the availability of petroleum products in the country as well as for neighboring land locked countries.

## TIPER'S CURRENT STORAGE CAPACITY BY PRODUCT IS SHOWN BELOW:


| Product | Capacity (Litres) |
|---|---|
| Diesel (AGO) | 180,246,000 |
| Premium Motor Spirit " (PMS) | 56,302,000 |
| Dual Purpose Kerosene (DPK) | 5,723,000 |
| HFO 180 | 11,383,000 |
| Total Storage Capacity | 253,654,000 |




# TIPER's future plan include:

- To increase the capacity by adding more tankage to facilitate the envisaged opera  tions of a special bonded warehouse and eventual Strategic Petroleum Reserve (SPR).
- Lifting the operating standards in all fronts especially the HSSEQ and attain the ISO certification.
- To gain validation in practical terms, to become the hub for petroleum supply chain for East and Southern Africa.
- Enhancing Truck Loading Operations to facilitate operational efficiency for Various customers.









# 4R ZAWA KIINI CHA MABADILIKO TANZANIA

Aidha, falsafa ya 4R imeimarisha shughuli za vyama vya siasa nchini pamoja na kufanya marekebisho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa ili kuimarisha mifumo ya uchaguzi. Vilevile imeimarisha diplomasia ya kimataifa.



Serikali imeendelea kutekeleza falsafa ya 4R iliyoasisiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Falsafa ya 4R ni ufupisho wa maneno manne ya lugha ya kiingereza yaani Reconciliation (Maridhiano), Resiliency (Ustahimilivu), Reform (Mabadiliko) na Rebuilding (Kujenga upya). Vilevile, falsafa hiyo ni mkakati mahususi unaolenga kuimarisha utawala bora, demokrasia na uchumi nchini, kwa kufungua milango ya mazungumzo na wadau mbalimbali wa kisiasa, kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na vyama vya siasa, asasi za kiraia na sekta binafsi.

Mafanikio yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa falsafa hiyo ni pamoja na kuundwa kwa tume mbalimbali ikiwemo Tume ya Haki Jinai, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi pamoja na Mifumo ya Usajili na Malalamiko ya ukiukwaji wa misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Tume ya Maboresho ya Kodi ili kutatua changamoto mbalimbali za wananchi pamoja na Kamati kwa ajili ya kutathmini utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili kuiwezesha Wizara kutekeleza malengo ya Serikali katika kukuza diplomasia ya uchumi na ushirikiano wa kimataifa.

Aidha, falsafa ya 4R imeimarisha shughuli za vyama vya siasa nchini pamoja na kufanya marekebisho ya sheria za uchaguzi na vyama vya siasa ili kuimarisha mifumo ya uchaguzi. Vilevile imeimarisha diplomasia ya kimataifa.

## UCHAGUZI WA HURU NA HAKI

Katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ambapo hadi Desemba 2024, kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kuboresha Daftari la wapiga kura katika mikoa 21 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo mikoa 16 ni ya Tanzania Bara na mikoa 5 ya Zanzibar; Kurekebisha taarifa za wapiga kura kupitia mtandao; Kuandikisha wafungwa katika magereza/wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na mahabusu.

Katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea na maandalizi ambapo hadi Desemba 2024, kazi zilizofanyika ni pamoja na: Kuboresha Daftari la wapiga kura

Utaratibu huu unafanyika kwa mara ya kwanza na utahusu wale waliohukumiwa na mahakama kifungo cha chini ya miezi sita gerezani au kwenye vyuo vya mafunzo. Vilevile, Tume imesambaza kwa wadau mbalimbali vikiwemo vyama vya siasa Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025 kwa ajili ya maoni na ushauri.

## UZEMBE KWENYE KUFUATILIA MIRADI YA MAENDELEO HAUPO

Katika kipindi chote cha utekelezaji wa Ilani, Serikali imeendelea kuimarisha uratibu wa ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo ili kuimarisha ufanisi, kupata thamani halisi ya fedha zinazotumika na hivyo kufikia malengo yaliyokusudiwa.
Katika kipindi hicho, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine wa kitaifa walifanya ziara na kutoa maelekezo, maoni na ushauri kwa ajili ya kuimarisha utendaji na utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Aidha, kwa mwaka 2024, mawaziri kupitia kauli mbiu ya "Rais Samia na Maendeleo, Wasikie na Waone" bila kujali sekta zao walifanya ziara mikoani ili kukagua, kuzindua, kuweka mawe ya msingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo na kufanya mikutano ya hadhara ili kuitambulisha miradi kwa wananchi na kuwafanya wananchi waone na wasikie mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na utendaji uliotukuka wa Rais wa awamu ya sita Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kutekelezwa kwa kauli mbiu hiyo kumechangia kuongeza kasi na ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mikoa yote nchini na kazi hii inaendelea.

# VISION PLUS
## YAITANGAZA TANZANIA IRAQ,YAFURAHISHWA

NA MWANDISHI WETU

Taasisi binafsi ya Vision Plus inayotoa huduma ya afya ya macho na miwani, imefanikiwa kuitangaza Kimataifa kutokana na kutoa huduma za kibingwa za macho nchini Iraq.

Hatua hiyo imewagusa wananchi wa nchi hiyo waliopatiwa huduma hiyo na taasisi hiyo ya Vision plus.

Akizungumza na jarida hili, Mtendaji Mkuu wa Vision Plus, Dkt. Hassanal Datoo alisena kuwa nafurahia kuitangaza kimataifa pamoja na kuwaeleza Wananchi wa Iraq kazi kubwa iliyofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Dkt. Datoo anasema ametekeleza dhamira yake hiyo pale alipopata nafasi ya kuhojiwa na maafisa wa ofisi ya Wqfu wa Kishia wenye makazi yake nchini Iraq ( ATABAT)

"Nilipata heshima ya kuhojiwa na maafisa kutoka ATABAT (Ofisi ya Waqfu wa Kishia – Iraq) hii ni Taasisi inayosimamia maeneo Matakatifu ya Kishia na kuratibu shughuli za mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's) wakati wa Arbaeen ya Imam Hussain.

"Pamoja na mambo mengine, lakinj mazungumzo yetu yalijikita katika mchango wangu kwa wa muda mrefu wa kuziwekea kambi za macho Zanzibar ambazo kwa miaka mingi nimekuwa nikitoa huduma za bure za matibabu ya macho kwa mahujaji na jamii za wenyeji wakati wa tukio hili takatifu.

"Ilikuwa ni heshima kubwa kuwasilisha maono yangu ya huduma na kuchunguza manufaa mapana ya mpango huu.

"Lakini pia kwa umuhimu mkubwa niliwapa historia fupi ya Zanzibar na maendeleo ya kasi yanayopatikana Tanzania na namna Rais Dkt. Samia anavyoleta maendeleo kwa kasi."








Vision Plus awali ilijulikana kwa jina ya Medical Eye Centre ilianzishwa mwaka 1979.






# NDANI YA UONGOZI WAKE

**AMEFANIKIWA KUSIMAMIA OMBI LA KUANDAA FAINALI ZA SOKA MATAIFA YA AFRIKA**

# AFCON 2027

Kuendelea na ukarabati wa viwanja vya Uhuru na Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam; kuendelea na ujenzi wa uwanja wa AFCON Arusha ambao



Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Michezo ¦Sports Academy¦ katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambao ume¦kia asilimia 10.

Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni nguzo muhimu katika ujenzi wa utambulisho wa kitaifa na mshikamano wa kijamii nchini. Katika kuimarisha sekta hii, Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo: kushirikisha shughuli za utamaduni, sanaa na michezo kuanzia shule za awali na msingi, sekondari na elimu ya juu.

Vilevile, kuhamasisha wananchi kushiriki michezo na mazoezi ya viungo vya mwili ili kuimarisha afya zao; kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kisasa katika sekta ya Michezo; na kutambua na kuendeleza vipaji vya vijana katika michezo kuanzia umri mdogo.
Kupitia mikakati hiyo masuala mbalimbali yametekelezwa kwa kipindi cha miaka minne kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha masuala ya habari kwa kufanya yafuatayo:
a) Kutoa taarifa ya uhakika na kwa urahisi zaidi kwa wananchi kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo ya kimkakati kupitia vipindi 50 vya KAZI IENDELEE vilivyorushwa kupitia Televisheni ya Taifa (TBC), majarida 5,000, machapisho 24,516 na jarida la miaka 60 ya Muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar;
b) Kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari kwa kusajili na kutoa leseni kwa magazeti 357, redio 215, televisheni 56, redio za mtandaoni 27 na televisheni mtandao 413;
c) Kuwezesha Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kufikisha matangazo yake katika nchi 16 za ukanda wa SADC. Vilevile, kuanzisha kipindi maalum kinachomulika masuala ya SADC kijulikanancho kama Eye On SADC; na
d) Kuzalisha ajira 20,919 ambapo wanaume ni 16,601 na wanawake ni 4,318.

ii. Kuimarisha, kusimamia na kueneza matumizi fasaha na sanifu ya Kiswahili ndani na nje ya nchi pamoja na kuendeleza shughuli za utamaduni kwa:
a) Kuongeza wigo wa misamiati ya Kiswahili ambapo maneno 1,274 ya lugha mbalimbali yamekusanywa;
b) Kutafsiri maandiko 7,548 ya lugha za kigeni kwenda Kiswahili na kutoka Kiswahili kwenda lugha za kigeni;
c) Kufanya tafiti tatu kuhusu lugha za asili na utamaduni usioshikika pamoja na tafiti tano zilizolenga kuongeza maneno kwenye Kongoo ya Kiswahili, hivyo, kuwezesha maneno 37,285,254 kuingizwa katika Kongoo la Kiswahili;
d) Kusajili vituo vipya 18 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni ambapo wageni 2,730 walinufaika;
e) Kuchapisha na kuboresha vitabu 16 vya kufundishia na kujifunzia Kiswahili kwa wageni;
f) Kuwezesha wataalamu 64 kupata ajira za kufundisha Kiswahili nje ya nchi;
g)Kutoa mafunzo kwa wataalamu 942 wa Kiswahili kuhusu mafunzo ya kufundisha Kiswahili kwa wageni;
h)Kutoa machapisho 333 ya kitaaluma na tafiti za kisayansi kwa lugha ya Kiswahili yakiwemo Jarida la Lugha Yetu Toleo Na. 40 (BAKITA); Kioo cha Lugha (UDSM); Mulika (UDSM); Kiswahili Katika Anga za Kimataifa (UDSM); na Nadharia za Elimu Mtindo ya Kiswahili;

i) Kuratibu mikutano ya kimataifa 56 iliyofanyiwa ukalimani kwa Kiswahili;
j) Kutambua na kuandika taarifa na kumbukumbu 5,000 za Urithi wa Ukombozi wa Afrika zinazoonekana na zisizoonekana; na
k) Kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotumia Kiswahili duniani kutoka watu milioni 190 mwaka 2020 na kufikia watu milioni 518 mwaka 2024.
iii. Kujenga mazingira wezeshi ya kukuza sanaa ikiwemo ngoma na bongo movie ili kufikia viwango vya kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo:

a) Kutoa mafunzo kwa wasanii 2,116 wa filamu kupitia programu za uchambuzi wa filamu, programu maalumu ya kuwaendeleza wasanii chipukizi pamoja na mafunzo kwa vitendo yalitolewa kwa wasanii wa filamu katika mikoa ya Dodoma, Geita na Dar es Salaam;
b) Kutoa leseni 1,633 kwa watumiaji wa kazi za ubunifu;
c) Kutoa vibali 667 kwa wasanii wa Tanzania kushiriki katika shughuli za sanaa nje ya nchi;
d) Kutoa vibali 205 kwa wadau wa sanaa kwa ajili ya kuingiza wasanii kutoka nje ya nchi ili wafanye shughuli za sanaa;
e) Kupokea, kuhakiki na kupanga filamu 5,114 katika madaraja pamoja na kuzipatia vibali vya usambazaji na uoneshwaji kwa umma;
f) Kusajili wasanii 3,369 katika fani tofauti za ubunifu kama filamu, muziki na maandishi;
g) Kukusanya na kugawa mirabaha yenye thamani ya jumla ya shilingi milioni 687.7 kwa wanufaika wa sanaa;
h) Kutoa mikopo yenye thamani shilingi bilioni 4.2 kwa wadau wa tasnia za sanaa na utamaduni muziki, filamu, maonesho na ufundi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 216;

i) Kutoa mafunzo mbalimbali ya sanaa na michezo kwa vijana 2,908 katika Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa); na
j) Kuzalisha jumla ya ajira 23,674 ambapo wanaume ni 10,302 na wanawake ni 13,372.
iv. Kuwawezesha wanamichezo washiriki kwenye mashindano mbalimbali, kuwatambua na kuwaenzi wanamichezo wanaofanya vizuri pamoja na kuimarisha miundombinu ya michezo kwa kutekeleza yafuatayo:
Kuhamasisha uanzishaji wa vilabu vya michezo 692, kusajili vilabu 115 vya mbio za polepole na kutoa vibali vya matukio 482 ya michezo ikiwemo mabonanza, mbio za polepole na marathon;

Kuendelea na ukarabati wa viwanja vya Uhuru na Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam; kuendelea na ujenzi wa uwanja wa AFCON Arusha ambao umefikia asilimia 16; kukamilisha ujenzi wa kiwanja kimoja cha KMC jijini Dar es Salaam na ukarabati wa viwanja viwili vilivyo katika shule za michezo za Tabora wavulana na Tabora wasichana; na Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Michezo (Sports Academy) katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambao umefikia asilimia 10.

# JOB NDUGAI 1963-2025




















KUTOKA KWA

MHARIRI MTENDAJI

# MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA IMEBEBA MAGEUZI

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Tanzania imeingia kwenye makubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo ja kugusa maisha ya wananchi na kuimarisha nafasi ya taifa kimataifa.

Tumeshuhudia kwenye miundombinu, kumefanyika miradi mikubwa iliyogusa maisha ya watu moja kwa. Moja baadhi yake ikiwa niujenzi wa barabara za kisasa, madaraja na reli ya kisasa ya SGR imepiga hatua kubwa, ikirahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria.

Audha sekta ya bandari imeboreshwa kwa uwekezaji mkubwa, kuongeza ushindani wa kibiashara katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Huduma za Afya zimeimarika kupitia ujenzi na ukarabati wa hospitali, vituo vya afya na upatikanaji wa vifaa tiba na vitendanishi huku elimu ikipata msukumo kupitia ujenzi wa shule mpya, ajira kwa walimu na programu za kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa elimu.

Katika maji, miradi mikubwa ya usambazaji imewafikia wananchi mijini na vijijini, ikipunguza adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Utalii umeimarishwa kwa kampeni ya “Royal Tour” na mikakati ya kuvutia watalii, ikipanua mapato na ajira.

Aidha kupitia falsafa ya 4R – Reconciliation, Resilience, Reforms, Rebuilding – Rais Dkt. Samia ameimarisha mshikamano wa kitaifa, kurejesha imani ya wananchi na washirika wa maendeleo.

Ukusanyaji wa kodi umeongezeka kupitia maboresho ya mifumo na uwazi wa TRA, huku fedha zikielekezwa moja kwa moja kwenye huduma za jamii.

Hakuna ubishi kuwa kipindi hiki kimeona uhuru wa habari na jukwaa huru la kisiasa vikipewa nafasi, jambo lililofungua ukurasa mpya wa majadiliano ya kimaendeleo kwa uwazi na heshima.

TZ&BEYOND tunaamininkuwa kwa ujumla, miaka minne ya Rais Samia imeweka msingi thabiti wa Tanzania yenye uchumi imara, wananchi wenye matumaini, na taifa linaloheshimika kimataifa.

Hii inamaanisha wazi kuwa wananchi wite wanalo jukumu la kuendeleza mshikamano huu kwa maendeleo endelevu



**Jimmy C. Kiango**
**MHARIRI MTENDAJI**



VISION PLUS EYE CLINIC
TIPER BULK STORAGE
TANZANIA REVENUE AUTHORITY ISO 9001: 2008 Certified
TIB CORPORATE BANK Your Partner Bank
KCB BANK
Air Tanzania The Wings of Kilimanjaro
CRDB BANK Tunakusikiliza
NSSF

## SHUKRANI
za dhati kwa WASHIRIKA WETU


Wananchi:
Oktoba
OCTOBER TUNATIKI


KCB
BANK
Tamba!
na KCB BIMA
Kata bima lipa kwa installment
mpaka miezi 10
Bima ya Gari
Bima ya Biashara
Bima ya nyumba
Bima ya Afya
Tamba!
na KCB BIMA
Heritage
Jubilee
www.kcbbank.co.tz